- SAFARI -



# RAFIKI SAFARINI

Kuwasaidia watu kuanza safari yao wenyewe

DIGNITY

www.dignityonline.org.uk

**Safari**
Kozi ya masomo ya Dignity

**Rafiki Safarini**

Toleo la Kwanza, 2020
Kiswhaili

**Ilani ya Hakimiliki na Sheria (Toleo la Kwanza, Oktoba 2020)**
Kazi hii kwa ujumla ni Hakimiliki © Dignity 2020 isipokuwa maeneo yaliyowekwa chini ya maandishi.

Mwandishi anazuia haki ya kudai bila kutuliza hakimiliki hii juu ya kazi zote za asili zilizomo ndani ya chapisho hili. Kazi hii inaweza kuzalishwa kwa ukamilifu na kusambazwa na Dignity (Ulimwenguni), Kampuni Iliyodhaminiwa kwa Dhamana. Imesajiliwa Uingereza na Wales No. 6394480. Chama cha Kusaidia No. 1122656.

Watu binafsi wanaruhusiwa kutoa nakala moja ya kazi hii kamili kwa matumizi yao binafsi. Maandishi ya kazi hii siku zote ni lazima kuchapisha kitabu kamili na haikubaliki kubadilishwa kwa namna yeyote. Hairuhusiwi kuchapishwa nakala nyingi.

Kama wewe ama shirika lako lingependa kuchapisha nakala nyingi kwa lengo la kusambaza, tafadhali wasiliana na Dignity uweze kupewa idhini. Gharama inaweza kuhitajika.

Kwa namna yeyote kazi hii hairuhusiwi kuchapisha nakala kwa lengo la kuuza na taasisi yeyote zaidi ya Dignity (Worldwide) Ltd.

Dignity
6 Barlow Moor Road
Didsbury
Manchester
M20 6TR
United Kingdom

Tovuti: hello@dignityonline.org.uk
No ya simu: +44 (0)7340 573 937

**Kikundi Kinachohusika na Safari**
Waandishi na Wahariri: Jon Paul Witt, Rebecca Burr, Ethan Witt na Jo Kimball
Msanii-Mchoraji na Mpangilio: Akash Sunny na Jo Kimball
Kusahihisha: Elisabeth Cartwright
Somo la 8: Kuomba kwa Pamoja ikijumuisha sehemu za asili iliyoandikwa na Sarah Small na Tobbias Ngala

**Vifungu vya Biblia**
Biblia Takatifu kwa Kiswahili, Muunganiko wa Vifungu, iliyochapishwa kama Biblia. Ilichapishwa kwa pamoja na Chama cha Biblia Tanzania, S.L.P. 175, DODOMA, Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya, P.O. Box 72983-00200, NAIROBI, Kenya.

**Taswira za Alama Zinazoongoza**
Taswira za Alama Zinazoongoza zimechorwa na Studio ya Metro Icon 5 iliyochapishwa na SyncFusion. Alama zimetumika kwa ruhusa.

# Yaliyomo

Kuhusu *Safari* .......... 1
Kuwasaidia watu kuanzisha *Safari* zao .......... 4
Namna watu watakavyotumia *Safari* .......... 7
Kuwa Rafiki .......... 10
Kuwa Kocha .......... 11
Kuwa mwanzilishi na Kuwasaidia Wengine kufanya Hivyo .......... 12
Kuunda *Safari* zaidi .......... 14
Utapata wapi msaada? .......... 15

# Kuhusu *Safari*

Mitume ni 'wale waliotumwa' wa kanisa la kwanza. Paulo na mitume wengine walichukua safari kubwa ya imani. Walipata njia ya kuwaeleza watu habari za ujumbe wa Yesu na kuchukua muda kuonyesha upendo na nguvu za Yesu kwenye jumuia na vijiji vingi. Hapo mwanzo waliwafundisha watu kuishi kwa kweli ya Yesu, wakisambaza ujumbe na matendo ya upendo wa Yesu kwao wenyewe. Haikuwahusu mitume wenyewe, iliwahusu watu wote.

Hapa ndipo unapohusika. Dignity imeanzisha ***Safari***, kozi ya kukusaidia kufuata hatua za wafuasi wa kwanza wa Yesu. Tunataka wewe ujifunze namna ya kuchukua hatua hizo wewe mwenyewe.

Kujifunza ***Safari*** itakupa wewe nafasi ya kujifunza kufanya kazi na Mungu, kuanzia kwenye kijiji chako au jumuia. Huhitaji kuhudhuria shule. Utajifunza mafundisho mahali pale pale ulipo, hata na marafiki wanaokuzunguka. Wakati kozi inapoendelea utawashirikisha watu ujumbe na upendo wa Yesu kila siku kwa wanakijiji na jumuia inayokuzunguka.

***Safari*** ni mtiririko wa mavipindi manne. Katika kila vipindi utajifunza namna ya kushiriki upendo na ujumbe wa Yesu kwa kuanzisha Vikundi vya Uzima au kuwasaidia wengine kufanya hivyo. Utaenda kwenye somo linalofuata wakati kazi ya matendo imekamilika. Tunataka kukuwezesha wewe kuanzisha kazi kwa matendo badala ya kujifunza tu neno la Mungu.

***Safari Kijijini*** inawasaidia watu binafsi kutambua hali iliopo sasa kwenye vijiji vyao na namna Kikundi cha Uzima inavyokuleta upendo wa Yesu na kujenga umoja. Watu binafsi watakuwa wameanzisha Kikundi cha Uzima mwisho wa vipindi hili.

***Safari ya Eneo*** inawasaidia watu binafsi kukua na kupanua kazi ya Vikundi vya Uzima kwa kuwahusisha wengine, hata kuanzisha Vikundi vya Uzima vingine. Watu binafsi watakuwa wamesaidia Kikundi cha Uzima kuanzisha kikundi kingine baada ya vipindi hili.

***Kuelekeza Safari*** hupeleleza namna ya kuanzisha Vikundi vya Uzima vipya kwenye maeneo mapya na watu wapya. Watu binafsi watakuwa wamewasaidia wengine kuanzisha Vikundi vya Uzima kwenye maeneo mapya mwisho wa vipindi hili.

***Kuongoza Safari*** husaidia watu binafsi kupata maono ya kwa ajili ya Vikundi vya Uzima kuanzishwa nchini kote. Watu binafsi watakuwa wamehusishwa katika kazi ya Heshima nchini kote mwisho wa vipindi hili.

# Kuwa Rafiki *Safarini*

Ndani ya Biblia kitabu cha Luka 24 tunakutana na hadithi ya Kleopa na rafiki yake wakitembea kuelea Emau. Hii ni safari ya kilometa 11. Wakati wanatembea walikuwa wakijadiliana juu ya matukio yaliyotokea siku iliyopita kuwa Yesu alikufa na fununu zikasikika kuwa 'amefufuka' tena. *"Walipokuwa wakizungumza na kujadiliana, Yesu mwenyewe akaja akatembea pamoja nao, lakini macho yao yakazuiliwa ili wasimtambue"* (Luka 24:15-16).

Yesu mwenyewe akaja na kuanza kutembea na hawa 'wafuasi' waliokuwa wamechanganyikiwa, na kuvunjika moyo na kuhitaji maelekezo. Walipokuwa wakitembea kwa pamoja aliwasikiliza, labda akawatania ili kutanua mjadala, wakijadiliana na kuendelea kutembea kwa pamoja kama mmoja wao. Walipokuwa wakitembea kwa pamoja Kleopa na rafiki yake waliuliza maswali na kujadili juu ya matukio yaliyotokea siku iliyopita. Yesu akajibu kwa kusema, *"Naye akianzia na Sheria ya Mose na Manabii wote, akawafafanulia jinsi Maandiko yalivyosema kumhusu yeye"* (Luka 24:27). Kwa maneno mengine, alichukua muda kumsaidia Kleopa na rafiki yake kuelewa alipokuwa akitembea nao.

Walipokaribia mwisho wa safari yao, Yesu aliendelea mbele. Kleopa na rafiki yake wakamsihi kwa bidii kubaki pamoja nao maana usiku ulikuwa umekaribia. Kama sehemu ya hii, wangekula na kuendelea kuwa na muda pamoja. Hiki ndicho kilichotokea: *"Alipokuwa mezani pamoja nao, akachukua mkate, akashukuru, akaumega, akaanza kuwagawia. Ndipo macho yao yakafumbuliwa, nao wakamtambua, naye akatoweka machoni pao. Hawakumwona tena. Wakaulizana wao kwa wao, "Je, mioyo yetu haikuwakawaka kwa furaha ndani yetu alipokuwa anazungumza nasi njiani na kutufafanulia Maandiko?"* (Luka 24:30-32).

Unaweza kusoma hadithi yote kwenye kitabu cha Luka 24:13-35.

Yesu alichukua muda kutembea na wafuasi waliyovunjika moyo. Aliwasikiliza, akaelewa tatizo lao akajadili pamoja nao. Akakaa pamoja nao akala chakula pamoja nao. Alipoumega mkate, walimtambua wakaelewa kila kitu alichokuwa akiwaambia.

Kuwa '***Rafiki Safarini***' humaanisha kufanya jambo hili kwa hao watu wanaojifunza Safari kwa ajili yao wenyewe. Wewe ni rafiki yao, kocha na mwanzilishi pia pamoja nao.

**Kuwa Rafiki**
Wewe ni rafiki tu kama wale marafiki wengine. Hivi ndivyo Yesu alivyotuonyesha kusaidia ufalme wake kukua. Uko hapo kutia moyo, kusikiliza, kupendekeza, kushauri na kusaidia. Marafiki wapo 'hapo' mmoja kwa mwingine. Mara nyingi ndani ya kanisa tunajaribu kutenda kama biashara, mahali watu wanakuwa mabosi au mabwana wakiwaambia wale walio chini yao nini cha kufanya. Hii siyo njia ya Yesu.

**Kuwa Kocha**
Mafundisho ya ***Safari*** inahusu kuanzisha Vikundi vya Uzima na kusaidia ufalme wa Mungu kukua ndani ya kijiji na ndani ya jumuiya. Kama mtu aliyekomaa na kujihusisha kuanzisha Kikundi cha Uzima mwenyewe, unao ujuzi wa kuwashirikisha wengine. Utakuwa umefanya uamuzi mkubwa na baadhi ya makosa pia. Ujuzi huu unakuwezesha kuwasaidia marafiki zako wasifanye makosa wenyewe na kujifunza kutokana na mambo mema yaliyotokea. Unapaswa kuwatia moyo wawe na imani katika Mungu, halisi kwa sababu umefanya hivyo.

**Kuwa Mtangulizi**
Mtangulizi maana yake ni 'kuanzisha vitu vipya.' Namna ya kutangulia, kuanzisha vitu vipya, ni kupitia wengine. Hii ndiyo mbinu aliyotumia Yesu, Mtume Paulo na wengine wasiyoweza kuhesabiwa katika historia yote ya kanisa. Yesu alikuwa rafiki kwa mitume wake na waliendelea kuanzisha kanisa. Paulo aliwainua wengi kibinafsi kwenye miji, jumuiya na vijiji kuzungumzia habari za Yesu. Inatupasa kufanya hivyo. Mara nyingi tunafikiri kuwa 'watu wa Mungu' wakubwa

ndiyo Mungu anafanya kazi kupitia wao. Tunaweza hata kujaribiwa kuamini kuwa sisi ni miongoni mwa 'watu hawa wenye nguvu, maalum' ambao ni zaidi ya watu wa kawaida. Hii siyo kweli. Mungu hufanya kazi kupitia mtu yeyote na kila mtu ndani ya ufalme wake. Kuwa mtendaji bora unapaswa kutembelea maeneo mengi kwa kuwawezesha, kuwaruhusu, kuwafundisha na kuwatia moyo wengine kufanya namna unavyofanya. Kwa njia hii utakuwa na hiki tunachokiita urithi. Ikifikia kuwa huwezi tena kufanya kazi, urithi uliyoacha utakuwa kwa watu wengi wakiendelea kufanya kazi. Itakuwa ni maelfu ya watu watakuwa wamempata Yesu na upendo kwa sababu ya tendo dogo ulilolifanya. Kamwe hutaweza kuelewa kitakachotokea kama matokeo ya hatua lakini itadumu. Hii ndiyo maana ya kutangulia.

# Kuwasaidia watu kuanzisha *Safari* zao

**Tunajaribu kufanya nini?**
Dignity inaamini kuwa Mungu hutumia watu ndani ya jumuiya zao kuwafundisha wengine habari za Yesu, kuwasaidia watu kwa matendo na kufanya kazi pamoja kuboresha maisha kwa kila mtu, hasa kwa watu masikini. Jambo moja ambalo haya yote yanategemea juu ya watu wake hasa watu waliyoitwa na Mungu kuleta tofauti.

Biblia inawazungumzia watu hao kuwa miti ya haki. Mivule ni miti mikubwa. Kifungu kinapatikana toka Isaya 61, hasa vifungu vine vya kwanza:

> 1 *Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu;*
> *kwa sababu BWANA amenitia mafuta*
> *niwahubiri wanyenyekevu habari njema;*
> *amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo,*
> *kuwatangazia mateka uhuru wao,*
> *na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.*
> 2 *Kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa,*
> *na siku ya kisasi cha Mungu wetu;*
> *kuwafariji wote waliao;*
> 3 *kuwaagizia hao waliao katika Sayuni,*
> *wapewe taji ya maua badala ya majivu,*
> *mafuta ya furaha badala ya maombolezo,*
> *vazi la sifa badala ya roho nzito;*
> *wapate kuitwa miti ya haki,*
> *iliyopandwa na BWANA, ili atukuzwe.*
> 4 *Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa,*
> *watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani,*
> *watatengeneza miji iliyoharibiwa,*
> *mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi.*

*Isaya 61:1-4*

Safari ambayo tungependa watu waanzishe ni safari pamoja na Mungu kuyafanya maneno haya ya Isaya kutokea ndani jumuiya zao. Mungu anataka watu hawa wawe mivule, miti mikubwa, ya haki. Hawa ni watu waliyopandwa na Mungu wanaoonyesha kila kitu kizuri kuhusu Mungu, atukuzwe.

**Namna ya kuwapata watu wliyo sahihi**
Watu wanaoanzisha ***Safari*** wakati mwingine ni watu unaowafahamu. Anaweza kuwa rafiki, au rafiki wa rafiki. Inaweza pia kuwa ni mtu uliyesikia habari zake kwenye eneo au mtu uliyemtembelea.

Kuna maswali mawili ya muhimu kumuuliza mtu anayependa kuanzisha ***Safari***. Swali la kwanza ni, 'Kwa nini wanataka kufanya?' na la pili ni, 'Wanaweza kufanya?' Maswali haya mawili yatatusaidia kufahamu kama Mungu amemwita mtu huyo kuanzisha ***Safari***.

**Kwa nini watu wanapenda kuanzisha *Safari*?**
Tuanze na swali, 'Kwa nini watu wanapenda kuanzisha ***Safari***?' Watu wanazo mitazamo tofauti, nyingine nzuri, nyingine mbaya na nyingine ni mchanganyiko wa zote mbili. Zaidi ya miaka ya kuanzisha Vikundi vya Uzima, tumewaona watu mbalimbali tofauti ambao wote wamekuwa na mitazamo tofauti. Hapa kuna baadhi ya mitazamo tuliyoona.

| Mfano wa mtazamo | Mzuri au Mbaya |
|---|---|
| Nataka mtui anipe vitu ili niweze kufanya hivi kuyafanya yafanane na mimi | ✖ |
| Nataka kusaidia kijiji changu | ✔ |
| Nataka kufahamu zaidi na kushuhudia habari za Yesu | ✔ |
| Nataka kuwaongoza watu | ✖ |
| Nataka kuwa ndani ya NGO, labda hii ndiyo njia bora ya maisha | ✖ |
| Nataka tu kusaidia watu | ✔ |
| Nataka kufanya yale ambayo Mungu anataka mimi nifanye | ✔ |

Kama utakuwa na uhusiano na mtu huyu, au kufahamu mtu aliyenae, utafahamu au kugundua mitazamo yao ni ipi. Hii inaitwa 'kuusoma moyo' wa mtu mwingine. Ikiwa hujamfahamu mtu vizuri, njia nzuri ya kuusoma moyo wa mtu huyo ni kuona yale anayojaribu kufanya bila kusaidiwa. Kama tayari wamekwishaanza kuwapenda wale wanaowazunguka bila msaada wowote, basi inaonekana kuwa wataendelea kufanya hivyo hata wakipata msaada.

**Je wanaweza kufanya *Safari*?**

Jambo lingine la kutazama ni kufikiri juu ya mtu anaweza kukamilisha kozi na kuanzisha Kikundi cha Uzima. Mungu huandaa mazingira ya maisha yetu kutuwezesha kufikia wito wake. Kwa mfano, kama mtu hawezi kusoma, itakuwa ni vigumu kwao moja kwa moja kuanzisha ***Safari***. Kama mtu hana mpangilio mzuri na maisha yao, mashamba au boma limejaa matatizo itakuwa ni vigumu sana kwao kuanzisha na kupangilia Kikundi cha Uzima au kuwasaidia wengine kwa yale wanayo kabiliana nayo.

Hii haina maana kusema watu hawa wametengwa. Hakika hapana! Hata hivyo, siyo bora, kuwa watu wa kwanza kuwaanza kwenye jumuiya au kijiji. Wakati mtu mmoja ama wawili wamejifunza ***Safari*** wenyewe na kuanzisha Kikundi cha Uzima, watu hawa wanaweza kuhusishwa na kusaidiwa. Kwa muda wanaweza hata kufanya wenyewe. Kwa mfano, mtu asijua kusoma anaweza kusaidiwa kujifunza kusoma! Ni vema kuomba ili Mungu na Roho wake Mtakatifu atatusaidia kuona watu sahihi wa kuwakaribisha na kufanya nao kazi.

Aina ingine ya mtu wa kumuepuka ni mtu mwenye shughuli nyingi mwenye kujishughulisha na kila kitu. Watu kama hawa wanaweza kuzungumzia mambo yaliyo sahihi lakini mara nyingi hawayazingatii na kufanya yale waliyoyakusudia kufanya. Kwa maana nyingine hawana muda!

Kwa watu, ikiwa utaweka mitazamao na nguvu zao pamoja kwa maombi, utapata wazo zuri kama ni mtu sahihi kwa wakati huu. Hii ndiyo Biblia inasema utambuzi na uongozi; kusema mabaya kutoka kwa mazuri, au njia mbaya kwa njia nzuri.

**Mtu anawezaje kuanzisha Safari?**

Waza kama unafikiri mtu Fulani ni mtu sahihi, kuna hatua fupi kwa watu kujisajili kwenye ***Safari***. Ni rahisi kufanya lakini ni muhimu sana kwa mtu anayejifunza kumaliza hatua hii wenyewe. Kujiunga nasi ni hatua ya kwanza kwenye safari na

kumtia moyo mtu kuchukua wenyewe itawasaidia kumiliki safari yao. Hawapaswi kukufanyia wewe ***Safari***, kanisa lao, Dignity au mtu yeyote mwingine. Hii ni hatua wanaotakiwa kuchukua wenyewe.

**Wanatakiwa kujaza fomu ya maulizo**

Hii ianatakiwa kurudishwa Dignity kwa **hello@dignityonline.org.uk** au wanaweza kupiga picha na kutumia WhatsApp au inayofanana na hiyo kutuma kwetu. Kama hawana mawasiliano kwa njia ya kisasa, watahitaji msaada wako kufisha fomu yao Dignity. Kwa mfano, unaweza kuwapa nakala ya fomu, waweze kujaza fomu, wakurudishie ili wewe uweze kutuma Dignity. Unawajibika kuwasaidia kuhusu hili. Kwa njia hii unaweza kuwa na mahusiano nao.

Unaweza kupata fomu ya maulizo kwa **www.dignityonline.org.uk/beginthejourney**.

**Tutadhibitisha kama watakuwa wamekubaliwa kwenye *Safari***

Tunawapokea watu waliodhibitishwa au walioomba kufanya kozi ya ***Safari***. Kawaida tunahitaji sababu za kumwelekeza mtu sehemu nyingine. Hata hivyo, ilivyo ni kwamba tunaweza kujisikia kuwa siyo mtu sahihi. Hatufanyi maamuzi haya wenyewe. Tutazungumza na wewe juu ya hilo kwanza.

**Nini basi kinatokea?**

Kwa tarehe maalum kwa mwaka mzima tunaanza ‘usajili’ mpya wa wanafunzi wa ***Safari***. Hii hutokea mara kwa mara hivyo watu hawapaswi kusubiri muda mrefu. Kwa kuanza nakala ya ***Safari Kijijini na Kitabu cha Kazi*** itatumwa kwa mtu anayefanya kozi. Kupunguza gharama na kutia moyo uwajibikaji tutafanya haya kwa njia ya mtandao tutakavyoweza, kupitia WhatsApp, email au njia nyingine. Hata hivyo tunafahamu kuwa kwenye maeneo maskini hii haiwezekani. Utakuwa pia na nakala ya vipindi na kitabu cha kazi. Kwa namna hii utaweza kutengeneza nakala na kumpa mtu anayesoma kozi hii. Unaweza kuchangia gharama za kufanay kazi hiyo mwenyewe kama utaweza. Kama hutaweza, Dignity watasaidia au wakati mwingine omba marafiki zetu kwenye maeneo mengine kupata msaada.

**Endelea kuwa rafiki, kocha na mwanzilishi**

Kama rafiki yeyote mwingine, unapaswa kuwasiliana na mtu anayefanya ***Safari***. Walao kila baada ya wiki 2 wasiliana nao ujue wanavyoendelea. Hasa, waulize wanaendeleaje na uwafuatilie kwa kazi fulani ambayo kila somo linawasisitiza wao kukamilisha. Kwa mfano, ndani ya ***Safari Kijijini***, hizi ni hatua anazopaswa mtu kuchukua hasa kuanzisha Kikundi cha Uzima. Tunao uhakika watakuwa na mapendekezo, maswali na mazingira ambayo unaweza kusaidia.

**Usidhani**

Usidhani tu kuwa mtu fulani anaendelea vizuri kama hujawasiliana nao. **Hakikisha wako sawa.** Katika mazingira mengine, kuanzisha Vikundi vya Uzima ni rahisi, na maeneo mengine ni ngumu sana. Tunapaswa kuwepo hapo kusaidiana.

# Namna watu watakavyotumia *Safari*

Kila vipindi ya ***Safari*** ina kusudi tofauti. Kila anayeanzisha ***Safari*** ni lazima aanze na ***Safari Kijijini***. Watu wataweza kuendelea na vipindi nyingine ikiwa na kama watamaliza kazi kwa matendo na umeridhika nayo. Katika kila hatua, watu wanajipatia uaminifu kwa kumaliza mafundisho na kazi za matendo ya ***Safari***.

| **Vipindi** | **Somo la kujifunzwa** | **Lengo na Sifa kwa vipindi inayofuata** |
|---|---|---|
| Safari Kijijini | • Ujumbe wa Yesu ni upi na ni namna gani utaueleza?<br>• Kikundi cha Uzima ni nini?<br>• Ni namna gani na kwa nini kuanzisha Kikundi cha Uzima<br>• Vipawa vya kujifunza vema na kufundisha vema<br>• Namna ya kumjua Mungu vema | • Anzisha Kikundi cha Uzima ndani ya kijiji chako au jumuiya yako. |
| Safari ya Eneo | • Vikundi vya Uzima na Kanisa<br>• Kuwapenda na kuwasaidia Maskini<br>• Kuanzisha Vikundi vya Uzima vingi kukuzunguka<br>• Namna ya kuwasaidia watu kufuata wito wa Mungu<br>• Mbinu za maombi, andaa na kuwatazama watu | • Kikundi cha Uzima chako kuanzisha Vikundi vya Uzima vingine kwenye vijiji vya karibu/jumuiya<br>• Unaanzisha kituo kidogo cha vikundi |
| Kuelekeza Safari | • Mpango wa Yesu ulikuwa ni upi?<br>• Kumfikia kila mmoja, hasa wale watu wa 'chini'<br>• Kuanzisha Vikundi vya Uzima kwenye maeneo mapya<br>• Mungu anatusaidia namna gani?<br>• Mbinu za kufundisha Biblia, kufanya kazi kama kikundi, kutambua na kujitazama mwenyewe kimwili na kiakili | • Nenda sehemu nyingine 'mpya' na kufundisha/wafundishe watu kuanzisha Vikundi vya Uzima wenyewe<br>• Unda kikundi kidogo kuendeleza mpango mbele |
| Kuongoza Safari | • Anzisha kwenye mikoa<br>• Vyanzo vya Dignity, mbinu na kufikiri<br>• Ndoto ya Mungu kwa mpango wetu ni upi?<br>• Kwenda kutoka 'maono' kuingia kwenye matendo<br>• Kujenga vikundi<br>• Utiwe ngumu na Roho<br>• Mbinukwenye umisheni wa mila<br>• Mbinu kwenye mitandao ya kijamii | • Anzisha kikundi kidogo uwafundishe somo la Dignity kwenye mikoa, vikundi vya watu au nchi |

**Vifaa vya mafundisho ni vipi?**

Kila vipindi ya ***Safari*** inajumlisha yafuatayo

- **Kitabu cha vipindi:** Hii inayo mafundisho yote na vifaa ambavyo mtu anayejifunza atahitaji kumaliza vyote.

- **Kitabu cha Kazi:** Hii inayo maswali, mazoezi na sehemu ya kufikiri kwa kila mtu. Itakuwa ni taarifa ya binafsi ambayo kila mtu amejifunza na yale ambayo Mungu ameongea nao na wanaweza kurudia kuvitazama.

<u>Vitabu hivyo viwili vinapaswa kupewanwa kwa pamoja siku zote.</u>
Kila mwanafunzi ni vema awe na Biblia na kalamu. Kama hawana Biblia tafadhali chukua hatua ya kuwawezesha wawe nazo. Unaweza pia kuwasiliana na Dignity kupata msaada kwa swala hili.

**Kuwasaidia watu kupata yaliyo bora toka *Safari***
Kila vipindi inayo masomo 10 ya kujifunza. Kila somo linapaswa kuchukua masaa 1.5 – 2. Inashauriwa kuwa mwanafunzi amalize moja kwa wiki. Kuna kazi ya matendo inayofuatana na kila somo. Wakati unawasiliana na mtu anayejifunza, mnaweza kujadili juu ya kazi hizo au maswali uone jinsi wanavyoendelea mbele.

Kitabu cha Kazi ni kwa ajili ya kila mwanafunzi kumaliza pamoja na kitabu cha mafundisho. Swali linapokuwepo au shughuli wanaweza kuandika majibu kwenye Kitabu cha Kazi. Wakishamaliza kila somo kuna maswali ya ziada na shughuli ndani ya Kitabu cha Kazi. Hii itawasaidia wao kufikiri kuhusu yale waliyoyajifunza, na kuingiza kwenye mazoezi na kupanua ufahamu wao. Ukimtembelea mtu, unaweza kupitia Kitabu chao cha Kazi pamoja nao, hii itasaidia wewe kufahamu hasa jinsi wanavyoendelea.

Ndani ya kila vipindi, yapo pia maandishi ya kumsaidia kila mwanafunzi kufikiri juu ya kufanya kazi (kuhudumia) pamoja na Mungu, kujenga mahusianao yao na Mungu au kuwapa wao taarifa. Kila andiko linaweza kuchukua muda wa dakika 30 kusoma na kulifikiria. Inayo maswali kuwasaidia wao kufikiri juu ya taarifa, mbinu au uongozi waliyosoma juu yake. Unaweza kutumia hizi kama alama kuwasaidia watu pia.

**Mifano na watu wa kujifunza kwao**
Kila somo linalo majibu na mawazo toka hadithi 3 'rafiki katika ***Safari***'. Kama mwanafunzi anayejifunza ***Safari*** watakuwa wanafuata maisha ya marafiki hawa watatu ambao wote wako kwenye hatua tofauti tofauti na ***Safari***. Watakuwa wanaanzisha Vikundi vya Uzima, wakifanya kazi kwenye vijiji vyao au kuwasaidia watu. 'Marafiki' hawa wako hapo kuwasaidia wanafunzi kuwatambua wale wanaojifunza kwao wanaokabiliana na maamuzi na mazingira hayo hayo. Kwa njia hiyo hiyo wataweza kusikia kutoka kwa hao 'marafiki', watakuwa pia wakisiliza kutoka kwako na watakuwa na maisha halisi ya kusimama nayo.

Hapa kuna tabia aina tatu tunayotumia kwenye ***Safari***. Yote yanatokana na mambo tofauti tofauti na kuwa na uelewe tofauti. Hawa ni watu wengi tofauti ambao unaweza kujihusisha nao.



**Agnes**
Agnes anaishi Kalambwa. Alijulishwa masomo ya Dignity na Fred binamu yake umbali wa km 500. Alijiunga na kozi ya ***Safari*** na kwa majuma amekuwa akijifunza Kikundi cha Uzima ni nini na kwa nini ni jambo jema kulianza. Ametamani sana kuanzisha kikundi na amezungumza na watu wengi. Amekuwa akiwasiliana na Julius anayeendesha kozi Zambia, na amekuwa akimtia moyo. Agnes na baadhi ya marafiki zake wako karibu kuanzisha Kikundi cha Uzima kwa wiki chache zijazo.



**Mutambo**
Mutambo ni kiongozi wa kanisa la High Faith nje ya Johannesburg, Africa ya Kusini. Anayo moyo wa kushawishi kanisa kuja pamoja na kufikia jumuia inayowazunguka. Amefanya ushirika na Dignity na amekuwa mtu wa kuunganisha huduma hii kwenye maeneo mengine. Amekuwa akiwasaidia kujifunza ***Safari Kijijini*** na ***Safari ya Eneo***. Mutambo alijifunza Vipindi hizi mwenyewe mwaka uliopita na alipozijifunza na kuingiza kwenye matendo alihamasika kuwasaidia wengine kufanya hivyo.



**Asisi**
Asisi anaishi Kenya na akaona kwenye mtandao matangazo ya Dignity. Kwa vile kozi ni bure alijisajili, akajifunza namna ya kuanzisha Kikundi cha Uzima akaenda kuvianzisha. Asisi amekuwa akijifunza namna na kuwatia moyo wengine kuanzisha vikundi pia. Wanapeleleza jinsi Kikundi cha Uzima vilivyopo vinaweza kuanzisha vingine na kuunda umoja. Anayo shauku kubwa kuona nini kitakachotokea.

**Kutumia *Safari* na kikundi**
***Safari*** imeandaliwa kwa mafundisho ya kibinafsi, hata ingawa inaweza kutumika na wengine kama kikundi. Unaweza kuwaza ndani ya utaratibu wa kijiji mahali ambapo wengi hawawezi kusoma na wenye elimu ndogo, hii inaweza kutumika.

Siku zote ni bora kwa mtu binafsi kumaliza kitabu wenyewe kabla hawajaanza na wengine toka kijijini au kwenye vijiji vingine. Kutumia utaratibu huu, watawasaidia wengine kufahamu namna wao na vikundi vyao walivyovianzisha kitaeneza upendo na ujumbe wa Yesu ndani ya vijiji vyao.

Kila mwisho wa kitabu cha vipindi, kuna sehemu inaitwa "***Kutumia Safari na Kikundi***" inayotoa mawazo na mwongozo wa kuongoza kila somo pamoja na kikundi.

# Kuwa Rafiki

Mmoja ya hadithi kubwa ya urafiki ndani ya Biblia ni Daudi na Jonathan. Unaweza kusoma hadithi yao kwenye kitabu cha 1 Samweli.

> *[1]Baada ya Daudi kumaliza kuongea na Sauli, roho ya Yonathani ikaambatana na roho ya Daudi, naye akampenda kama nafsi yake mwenyewe. [2]Kuanzia siku ile Sauli akamchukua Daudi naye hakumruhusu kurudi nyumbani kwa baba yake. [3]Yonathani akafanya agano na Daudi kwa sababu alimpenda kama nafsi yake mwenyewe. [4]Yonathani akavua joho alilokuwa amevaa na kumpa Daudi, pamoja na koti lake, silaha zake, hata pamoja na upanga wake, upinde wake na mshipi wake.*
>
> *1 Samweli 18:1-4*

Tunapaswa kuwa marafiki na hao wanaojifunza ***Safari***, kama Jonathan na Daudi.

Urafiki labda ni mmoja ya kitu kikubwa cha kutia moyo ambayo Mungu amefanya. Kufanya kazi kwa pamoja kwenye ufalme wa Mungu na marafiki wakubwa hivyo ndivyo ilivyokusudiwa kuwa. Tunaitwa ndugu na dada kwa sababu. Ufalme wa Mungu ni familia ya marafiki. Hii ndiyo sababu tunazungumzia kuwa 'kiongozi' au kuwa na 'kaimu' au nafasi yeyote au sifa fulani haisaidii kitu chochote. Haya yalitokea wakati wote wa kuendeleza kanisa na ni makosa! Sisi tuu marafiki na wana familia.

Hapa kuna baadhi ya mambo ya kufanya kusaidia jambo hili:

- **Muwe na muda pamoja na kutembeleana:** Tumia muda wa kawaida na watu wanaofanya ***Safari***. Unaweza kufanya jambo hili kama wewe, kwa simu, kutuma ujumbe kwa WhatsApp au hata barua. Urafiki wenu utasababisha dunia tofauti ya mafanikio au kushindwa.
- **Kutia moyo:** zungumza maneno ya kutia moyo kwa marafiki zako na uwaulize wanaendeleaje. Furahia yale wanayoyafanya na namna unaweza kuwasisitiza kusonga mbele.
- **Sikiliza:** Wasikilize na historia zao. Inawezekana wanayo furaha au magumu. Hali yeyote ile, wasikilize. Usiwe mwepesi wa kuongea.
- **Uwepo hapo:** Weka agano la 'kuwepo hapo' na 'ujihusishe'.
- **Fanya kitu cha kufurahisha:** Unapomwona mtu huyo uwe na wakati wa kafanya jambo lolote la kufurahisha na ushirikiane nao. Hayo yote ndiyo urafiki hufanya!
- **Omba:** Waombee kila wakati.

**Urafiki wako huwaweka watu kufikia malengo yao ambayo Mungu anayo kwa ajili yao.**

# Kuwa Kocha

Kama kwenye michezo mfano mchezo wa mpira au mpira wa mezani kila timu au mchezaji anayo kocha. Kocha ni mtu anayetoa maelekezo na mwongozo kwenye timu au kwa mchezaji bora. Mungu ametupa uwezo wa kuwa 'kocha' kwa watu wanaojifunza ***Safari***, kuanzisha Vikundi vya Uzima, kuwasaidia wengine kufanya hivyo au wanatumikia jumuiya zao. Hili siyo jambo jipya, ilitokea kwenye kanisa la kwanza pia. Tunaona mahusiano kama hayo kati Paulo na Timoteo kwenye 2 Timoteo sura ya 4.

> *1 Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu watu walio hai na waliokufa wakati wa kuja kwake na ufalme wake, kwamba: 2 Hubiri Neno; kuwa tayari wakati ufaao na wakati usiofaa; karipia, kemea na utie moyo kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho mazuri… 5 Kwa habari yako wewe, vumilia mateso, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza wajibu wote wa huduma yako.*
>
> *2 Timoteo 4:1-2 & 5*

Wajibu wako ni 'kukochi' hao wanaojifunza ***Safari*** siyo tu kuendelea na kumaliza masomo ila waweke kwenye mazoezi pia. Kila mara tunapochukua hatua kufanya kazi ya Mungu, mara zote kunakuwepo na maswali na matatizo. Ujuzi ambao umekuwa nao utakuwa ni wa dhamani pale mtu mwingine anapojifunza kutoka kwako. Hii haina maana kuwa utakuwa na majibu wakati wote. Wakati mwingine kuzungumzia juu ya shida au kuiona kwa mtazamo mwingine inasaidia. Hii ndiyo maana ya kumkochi mwingine.

Ni muhimu sana usifanyike 'bwana' juu ya mtu yeyote au kuwa msimamizi. Kila mtu anapaswa kuwa huru kufanya makosa yao wenyewe na kufanya maamuzi yao wenyewe. Uko hapo kuambatana nao, siyo kuwaambia jambo la kufanya.

Hapa kuna baadhi ya maeneo ambayo unaweza kufundisha:

- **Elezea Biblia/mafundisho:** Watu wengine wanaojifunza ***Safari*** wanaweza wakahitaji baadhi ya maelezo ya mafundisho, fikra nyuma yake au maswali mengine. Unaweza ukatoa hii.
- **Maelekezo na Hekima:** Inaweza ikawepo shida inayomkabili mtu anayejifunza. Kwa mfano, labda watu wengi kwenye jumuiya zao wanapingwa kwa yale wanaojaribu kufanya au labda kila mmoja amegawanyika. Ujuzi wako uliyopita au masomo uliyojifunza inaweza kuwasaidia wao.
- **Ujuzi:** Ujuzi ni yale uliyoyajifunza kwa nyakati. Unaweza kutoa ujuzi wa elimu yako kwa wale wanaojifunza ***Safari*** na kuanzisha Vikundi vya Uzima.
- **Muda:** Kutoa muda wako kwa mtu unayemfundisha ni kitu cha dhamani sana. Lengo lako ni kuwasaidia wao kupata majibu wenyewe, na siyo lazima kuwaambia jambo la kufanya!
- **Mbinu:** Watu wengine wanaowafundisha hao kupitia ***Safari*** watakuwa wamejifanyia vitu kabla ya wao wenyewe. Watakuwa wameona jinsi Vikundi vya Uzima vinavyokua na kusaidia jumuiya zao. Labda wameshaanzisha Vikundi vya Uzima vingine na kuanzisha vituo. Unaweza kuwasaidia kwa kuwaelekeza njia sahihi ya kufikiri. Njia sahihi siku zote ni kuwaamini na kuwawezesha.
- **Onyo kwa hatari:** Labda mtu ameharibika upande fulani. Labda unaweza kuwasaidia kutambua hilo. Labda mazingira ndani ya vijiji vyao inaweza ikawa mbaya kwa urahisi nao ni vipofu kwa jambo hilo. Kukuwepo hatari yeyote, utaweza kusikiliza na kutoa hekima kiasi ya namna ya kukwepa hatari hiyo.

**Lengo lako la kuwa kocha ni kuwasaidia watu kufanya mambo sahihi kwa uwelewa ili waweze kuyafikia malengo yao.**

# Kuwa mwanzilishi na Kuwasaidia Wengine kufanya Hivyo

Mwanzo wa kitabu hiki tulizungumzia juu ya tabia ya kuwa mwanzilishi ni ili kwamba watu warithi maisha yale uliyoyaishi wewe. Kazi ya Dignity siyo kwamba wewe ufanye kila kitu na kuwa 'mtu' mkubwa au 'mwanamke' wa Mungu. Haya siyo mambo ambayo Mungu anahitaji kwetu. Mfano wa Yesu ni kutufanya sisi kutokuwa lolote na kuwaruhusu wengine kuishi na kustawi. Ndiyo, unaweza ukawapata watu wa kujifunza kozi ya ***Safari***, kuanzisha Vikundi vya Uzima mwenyewe na kufanya kila unachoweza kufanya. Hata hivyo, utakuwa mtendaji bora kama utawawezesha wengine kuanzisha pia. Tunaona kuwa Mtume Paulo alifanya haya na Priskila na Aquila na kwa wakati wakamsaidia pia mtu anayeitwa Apollo kufanya hayo.

> *18Baada ya kukaa Korintho kwa muda, Paulo akaagana na wale ndugu walioamini, akasafiri kwa njia ya bahari kwenda Shamu akiwa amefuatana na Prisila na Akila. Walipofika Kenkrea, Paulo alinyoa nywele zake kwa kuwa alikuwa ameweka nadhiri. 19Walipofika Efeso, Paulo aliwaacha Prisila na Akila huko, lakini yeye akaingia kwenye sinagogi akawa anajadiliana na Wayahudi.*
>
> *Matendo 18:18-19*
>
> *24Basi akaja Efeso Myahudi mmoja, jina lake Apolo, mwenyeji wa Iskanderia. Yeye alikuwa na elimu kubwa, pia alikuwa hodari katika Maandiko. 25Alikuwa amefundishwa katika njia ya Bwana, naye alikuwa na bidii katika roho, akafundisha kwa usahihi juu ya Yesu, ingawa alijua tu ubatizo wa Yohana. 26Apolo alianza kunena kwa ujasiri mkubwa katika sinagogi. Lakini Prisila na Akila walipomsikia, walimchukua kando na kumweleza njia ya Mungu kwa ufasaha zaidi.*
>
> *27Naye Apolo alipotaka kwenda Akaya, ndugu wa Efeso walimtia moyo, wakawaandikia wanafunzi huko ili wamkaribishe. Alipofika huko, aliwasaidia sana wale ambao, kwa neema ya Mungu, walikuwa wameamini. 28Kwa uwezo mkubwa aliwakanusha hadharani Wayahudi waliokuwa wakipinga, akionyesha kwa njia ya Maandiko kwamba Yesu ndiye Kristo.*
>
> *Matendo 18:24-28*

**Nguvu ya watu**

Paulo alifanya kazi na Priskila na Aquila na kuwaacha Efeso. Huko walikutana na mtu anayeitwa Apollo aliyehitaji msaada na kutiwa moyo. Akaenda Akaya akawa msaada mkubwa sana kwa ndugu waliokuwa huko.

Hii yote ilianza na mtu mmoja Paulo aliyemwamini Priskila na Aquila ambao nao walimwamini Apollo. Matendo ya Paulo yalimalizikia kugusa maeneo matatu tofauti kwa injili ya Yesu. Tunapaswa kufanya hivyo! Isingeliwezekana kwa Paulo kuanzisha huduma maeneo yote. Alitambua hilo, hivyo alifundisha vikundi vya marafiki kuwa waanzilishi. Aliwatia moyo kufanya hivyo.

Tunapaswa kufanya hivyo. Mtume Paulo hakusafiri kila mahali injili ilkofikia, lakini kwa sababu yake, maeneo mengi yalifikia kufahamu ujumbe, kweli na upendo wa Yesu.

**Tengeneza Jumuiya ya Watangulizi**

Unaweza kuwa rafiki kwa hawa watangulizi wote na unaweza hata kuwa kocha wao. Jambo linalowajibisha hasa ni pale unapowasaidia kufanyika hivyo moja kwa mwingine. Unaunda jumuiya ya watangulizi. Kufanya mkusanyiko mara chache kwa mwaka au kuwa na kikundi cha WhatApp ni njia bora ya kutia moyo jambo hilo. Hii itawasaidia watu kujifunza mtu kwa mwingine. Hii inaweza kusaidia kazi kwa kufundisha watu juu ya Yesu na pia kushirikisha elimu ya matendo ya namna ya kuwasaidia watu ndani ya kijiji.

**Kuunganisha watu wa Dignity kwa upana**

Vyanzo vingi na na msaada vinapatikana. Unaweza kuwatia watu wote moyo uliyowatangulia kuunganika na Dignity. Kwa njia hii wanaweza kuombewa na kutiwa moyo.

**Omba**

Waombee wote!

Lengo lako ni kuwatia watu moyo kujifunza ***Safari*** wawe watangulizi ili wao kufanya hivyo sawa na watu wanaowafahamu. Kwa namna hiyo utakuwepo kila 'mahali' lakini kamwe hajawahi kukanyaga maeneo hayo unayoyaendeleza.

# Kuunda *Safari* zaidi

Unaposoma haya, utakuwa unawasaidia watu kujifunza kozi ***Safari*** wao wenyewe. Watakuwa wakianzisha Vikundi vya Uzima, baadhi ya watu watakuwa wakisaidia jumuiya, na wengine watakuwa wakifundisha habari za Yesu. Haya yote ni mambo makubwa!

Watu watakapokuwa wamefika mwisho wa ***Safari Kijijini***, watahitajika kuanzisha Kikundi cha Uzima kuhitimu kwa ***Safari ya Maeneo***. Mwisho wa vipindi ya pili huyo mtu na Kikundi chao cha Uzima watapaswa kuanzisha Vikundi vya Uzima vingine kwa ajili yao wenyewe. Kama sehemu ya jambo hili watahitajika kuonyesha matendo ya upendo wa Yesu ndani ya kijiji chao.

Watakuwepo watu ambao wewe, au hao wanaojifunza ***Safari***, watakutana na watu wazuri wa kuanzisha Kikundi cha Uzima. Wewe pamoja na watu hao wanaojifunza ***Safari*** mnaweza kuwateuwa miongoni mwa watu hawa kujifunza ***Safari*** wenyewe.

Kufanya hivyo, wasiliana na Dignity au Yule mtu wa mawasiliano moja kwa moja.

Pia panaweza kuwepo maeneo ambayo hakuna Vikundi vya Uzima vinavyoendelea nawe unapenda viwepo! Njia kuu ya kuanzisha ni kuwatembelea, na kuwatafuta baadhi ya watu ambao unadhani Mungu anawaita na kuwakaribisha wao kujifunza ***Safari*** wenyewe. Hatupendi kitu zaidi ya kukusaidia wewe na watu wengine kufanya jambo hili.

Kwa njia nyingine ni rahisi…

...Watu zaidi wa kujifunza ***Safari***…

…Watu zaidi wa kuanzisha Vikundi vya Uzima…

…Watu zaidi wa kujifunza habari za Yesu ndani ya Vikundi vya Uzima

…Maisha zaidi yamebadilishwa!

Maisha zaidi kubadiliswa maana yake ni upendo zaidi, msaada na kweli ndani ya kijiji…

…Hii ina maana kumhitaji Yesu zaidi na maisha bora kwa kila mmoja…

…Hii ina maana watu zaidi wa kujifunza ***Safari***…

…na endelea kuanzisha vikundi zaidi na zaidi watakaofanya hivyo.

**Hivi ndivyo tunavyobadilisha maisha ya wengi, watu wengi kuwa bora, hasa hao ambao ni maskini.**

**Je kuna mtu yeyote unayemfahamu wa kuanza Safari yake leo? Tujulishe!**

# Utapata wapi msaada?

Kunazo njia chache ambazo unaweza kupata msaada na kutegemezwa. Kama una swali, mambo ya kutia moyo, shuhuda kubwa au kukabiliana na tatizo, wasiliana nasi. Usitunze mwenyewe!

**Kwa kuunganika na wengine ambao ni '*Marafiki kwenye Safari*'**
Siyo wewe pekee ndiye mtu anayewatia wengine moyo kuanzisha na kuendelea na ***Safari*** zao. Kuna wengi kwenye mataifa mengine wakifanya hivyo pia. Tutakuunganisha na watu hao kupitia WhatsApp na ni sehemu kubwa ya kupata mwongozo, saidia au hata mtu mmoja wa kumwombea.

**Kwa kuunganika na mtu wako wa mawasiliano wa Dignity**
Utakuwa na mawasiliano na mtu wa Dignity anayejulikana na wewe ndani ya nchi yako ama nje ya nchi. Wasiliana na mtu huyo nao watawasiliana na wewe. Huyo ni mtu bora wa kumwendea kwa msaada na kwa maelekezo.

**Kwa kuunganika na Dignity ndani ya UK**
Unaweza kuwasiliana na Dignity moja kwa moja kwa kututumia email hello@dignityonline.org.uk au unaweza kutumia WhatsApp yetu ya kimataifa +447340573937.

**Kwa maombi**
Hii inaweza kuwa wazi kusema – lakini tutasema hata hivyo! Kuna baadhi ya mazingira ambayo ni magumu, tunafahamu hivyo. Mara zote nenda kwa Mungu Baba kwa njia ya Yesu Kristo kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Saa zote Yupo hapo kuingilia.

**Tuwasiliane! Tunataka kukusaidia kwa kadri tutakavyoweza kuwa rafiki kwenye safari kwa wengine. Tuko hapa kwa ajili yako!**

Wasiliana nasi kwa **hello@dignityonline.org.uk** au **+447340573937**.
Kwa mtiririko wa vitabu vyetu na bei tembelea mtandao wetu:
**www.dignityonline.org.uk/publications**

Swahili Toleo la Kwanza

© Dignity. Dignity chama cha kusaidia kilichosajiliwa no. 1122656.
Dignity (Worldwide) ni kampuni iliyodhibitiwa na dhamana,
iliyosajiliwa Uingereza na Wales no 6394480.